Chama Cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu
P.O. Box 11727, Dar Es Salaam
http://thtu.biz.tc/, katibu@thtu.biz.tc, mobile: 0755 576 224

# MUHTASARI WA AGENDA ZA KIKAO NA WAZIRI MKUU

1. **Umuhimu wa kuwahamishia wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii ulio bora zaidi ya PPF, NSSF na SSSS**

**Hoja 1.1:** Tafiti zimeonyesha kuwa Mfuko wa hifadhi ya Jamii wa PPF unawadhulumu sana wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu na mfuko huo hauko tayari kufanya marekebisho ya kuboresha mafao kwa wastaafu. Aidha wafanyakazi wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu hulipwa mishahara na serikali hivyo hawana tofauti kubwa na wafanyakazi wa serikali. Aidha wafanyakazi waliopo kwenye skimu ya SSSS wanadhulumiwa haki zao kwani skimu hiyo haikidhi matakwa ya mifuko ya hifadhi ya jamii. Viongozi wa Wanataaluma na Wafanyakazi waendeshaji walipeleka mapendekezo kwa Wizara ya Elimu na Ufundi kuomba wahamishiwe kwenye mfuko wenye mafao bora ya uzeeni au mifuko ya PPF na NSSF iboreshwe ifikapo January 2009.

**Pendekezo1.1:** Serikali iharakishe taratibu za kuwahamisha wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu kutoka PPF kwenda kwenye mfuko ulio bora zaidi ya PPF.

**Pendekezo1.2:** Serikali iwahamishie wafanyakazi waliokuwa katika skimu ya SSSS kwenye mfuko wa jamii ulio bora haraka iwezekanavyo.

**Pendekezo1.3:** Serikali iweke utaratibu ambao unahakikisha mafao ya uzeeni yanajumuisha thamani halisi ya mchango wa mwajiri na mwajiriwa kwa kufanya marekebisho ya anguko la thamani ya fedha na mfumuko wa bei toka mifuko hiyo ianzishwe.

2. **Haja ya kuboresha mishahara ya wafanyakazi wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu ili ikidhi mahitaji halisi ya wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu.**

**Hoja 2.1:** Maendeleo ya kweli ya taifa yanasukumwa na wasomi na wataalam walioko katika sekta mbalimbali za maendeleo ambao kwa idadi hawazidi asilimia mbili ya idadi ya watu wa Tanzania. Ongezeko kubwa la gharama za maisha katika kipindi cha miaka mitano iliyopita limefuta kabisa nafuu waliyopata wasomi na wataalam wa nchi yetu kutokana na ongezeko la mishahara ya wanataaluma lililofanyika mwaka 2006/2007. Aidha wafanyakazi waendeshaji wengi katika taasisi za elimu ya juu hawakupata ongezeko ambalo serikali iliridhia katika pendekezo la Kamati ya Rais ya 2005. Wafanyakazi wengi pia hawajalipwa marupurupu stahili ikiwa ni pamoja na muda wa ziada kazini, pango, usafiri na kadhalika. Aidha wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu wamebebeshwa mzigo mkubwa sana wa kodi ukilinganisha na wafanya biashara.

**Hoja 2.2: "**Government standing orders; standing orders for the public service 1971, section m, m.1-2" zinaeleza wazi kuwa kazi za ualimu ni mojawapo ya makundi ya kazi ambazo ni kazi maalumu "special services" ambazo waajiriwa wake wanastahili kupewa nyumba. Lakini swala la nyumba kwa wanataaluma na waendeshaji wa taasisi za elimu ya juu limekuwa ni tete hasa ukizingatia kuwa mwajiri anaambiwa alipe posho ya nyumba kutoka OC ambayo mara nyingi haitoshi. Kwa wale wafanyakazi ambao ni wanataaluma tatizo la nyumba linakuwa ni kikwazo kikubwa kwao kufikia upeo wa ufanisi hasa ikizingatiwa kuwa kazi za mwalimu haziishi anapotoka ofisini bali huendelea kutoa huduma kama vile maandalizi ya vipindi, kusahihisha mitihani na kufanya tafiti akiwa nyumbani. Hivyo nyumba yake ni ofisi mbadala wakati akiwa nyumbani. Aidha pale ambapo posho ya nyumba inatolewa TRA nayo inadai kodi kana kwamba fedha hiyo imetolewa kwa matumizi ya kawaida na sio kulipia pango.

**Pendekezo 2.1:** Serikali itekeleze ahadi yake ya kuwalipa wafanyakazi wote waendeshaji mishahara iliyopendekezwa na kamati ya Rais ya 2005 pamoja na posho na marupurupu yao.

**Pendekezo 2.2:** Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya mishahara mipya inayokidhi hali na mazingira ya sasa ya gharama za maisha hasa ukizingatia kuwa hata lile pendekezo la mishahara la 2004 na 1994 halikulipwa kikamilifu.

**Pendekezo 2.3:** Serikali iweke utaratibu wa kutoa posho ya nyumba na usafiri kwa wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu ili kuboresha mazingira ya kazi na kuongeza ufanisi kazini na kuhakikisha vyuo vinazalisha rasilmali watu bora.

**Pendekezo 2.4:** Sheria ya kodi ya mwaka 2004 iangaliwe upya ili kuondoa vifungu ambavyo vinavyoagiza kodi ikatwe kutoka kwenye mafao maalum kama vile mafao ya uzeeni, posho ya nyumba na kadhalika. Aidha serikali iangalie uwezekano wa kupunguza kodi ya "lipa kama upatavyo" (PAYE) ambayo ni kubwa mno ukilinganisha na kodi inayolipwa na wafanyabiashara.

**Pendekezo 2.5:**Serikali iangalie jinsi ya kupunguza kodi ya PAYE kwani kodi hii ni kubwa mno kwa wafanyakazi.

**Pendekezo 2.6:** Deni la posho ya nyumba kwa wafanyakazi wanaostahili lilipwe. Pia serikali iangalie utaratibu wa kuwalipa wafanyakazi wote posho ya nyumba na usafiri.

## 3. Kuondoa tofauti kubwa za uwezeshwaji wa taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu vya serikali

**Hoja 3.1:** Kuna tofauti kubwa ya Muundo, Usimamizi na Uwezeshwaji wa Taasisi za elimu ya Juu na Vyuo Vikuu kwa sababu vyombo hivi vinapatikana katika makundi tofauti: Taasisi na Vyuo vya Umma, Taasisi na Vyuo vya Sekta za Wizara mbalimbali. Kwa sababu hii kunakuwa na tofauti kubwa za ki-muundo, ki-usimamizi, na ki-uwezeshwaji wa taasisi na vyuo vikuu. Pamoja na tofauti hizi taasisi na vyuo hivyo vyote vina jukumu moja tu la kuandaa rasilmali watu bora ya taifa kwa ajili ya maendeleo yetu. Aidha maamuzi ya serikali ya kuchanganya elimu ya juu na elimu ya msingi katika wizara moja yalifanywa

kwa haraka bila kuangalia kwa makini na kwa upana mazingira ya sasa na athari zinazoweza kujitokeza kufuatia kupanuka kwa kasi kwa idadi ya shule za misingi, sekondari, na taasisi za elimu ya juu.

**Pendekezo 3.1:** Serikali iliangalie swala hili upya kwa kuzingatia kipaumbele cha Elimu na mahitaji halisi ya elimu ya Juu nchini. Aidha kuna umuhimu wa kutenganisha sekta ya elimu ya juu na sekta ya elimu ya msingi/sekondari ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji.

**4. Kuweka utaratibu wa kusimamia taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu binafsi.**

**Hoja 4.1:** Taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu binafsi navyo vinafanya kazi ya kuandaa rasilmali watu bora kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu. Aidha japokuwa TCU na NACTE ni vyombo vyenye mamlaka ya kusajili na kufuta vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu serikali haina njia madhubuti za kudhibiti ubora wa mitaala katika vyuo hivyo. Iko haja ya kuweka uwiano wa mitaala inayofanana katika taasisi hizo na zile za serikali. Aidha Vyuo hivyo hupata ruzuku kupitia mamlaka ya mikopo ya elimu na hivyo ni vyema serikali ikajipa nafasi ya kuvisimamia vyema kuhakikisha fedha hiyo inatumika vyema kwa maendeleo ya taifa.

**Pendekezo 4.1:** Serikali iweke utaratibu mzuri wa kusimamia taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu binafsi ili vitoe rasilmali watu walio katika viwango vinavyokubalika sambamba na vile vya umma.

**5. Kuboresha na kuunda taasisi za elimu ngazi mbalimbali bila kuua zilizopo.**

**Hoja 5.1:** Katika kipindi cha hivi karibuni taasisi nyingi zilizokuwa zinatoa vyeti na shahada za ufundi, utaalamu ngazi mbalimbali zimepokwa na kufanywa vyuo vikuu au vyuo vikuu vishiriki. Kukosekana kwa ngazi hizi za kati na chini kunaathiri maendeleo ya Taifa kwani wahandisi, wauguzi na wataalam wanaotoka vyuo vikuu hawawezi kufanya kazi zao bila msaada wa hizo kada za kati na chini. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais aliliona tatizo hili na akaagiza utaratibu huo usitishwe.

**Pendekezo 5.1:** Kuna haja ya kurejesha zile taasisi zilizobadilishwa kwa kuziunda upya ili zitoe huduma ya kuwaandaa wataalam na mafundi mchundo/wasaidizi na wahandisi wasaidizi watakaofanya kazi na wale waliomaliza shahada ya juu kwa kuwa asili mia kubwa ya maendeleo ya nchi yanategemea nguvu kazi yenye elimu yakati ikiongozwa na wale wenye shahada ya juu.

**Hoja 5.2:** Kufuatia wimbi la utandawazi mitaala bora ya nchi yetu ya zamani kama vile FTC ambayo ilichangia kikubwa maendeleo ya nchi hii miaka ya mwanzo ya Uhuru ilifutwa au kuwekwa kando. Dhana potofu ya kwenda na wakati ilitumika kufuta yale mazuri tuliyoyaunda sisi wenyewe kwa kuthamini zaidi mambo ya mpito ambayo yaliletwa na wimbi la utandawazi. Imani kuwa kulandana na mambo ya utandawazi ndiyo njia ya kujikwamua kiuchumi na kielimu ni potofu kwani historia inatufunza kuwa kila mgeni aliyekuja Tanzania alikuja na hila za kupata yeye na kutukosesha sisi ili mradi tu mwanaye ale mkate kwa siagi wakati wa kwetu anakufa kwa utapia mlo.

**Pendekezo 5.2:** Katika miaka ijayo kabla ya serikali kuleta mabadiliko ya sera au sheria zinazosimamia elimu au sekta nyingine muhimu za nchi, ifanye jitihada za dhati kuwatumia watafiti wazalendo ambao wanaelewa fika historia, hali na mazingira ya taifa letu ili sera na sheria zilinufaishe taifa la Tanzania pamoja na vizazi vijavyo.

**Hoja 5.3 :** Mitaala iliyopo katika taasisi mbalimbali za elimu ya juu inatofautiana mno na kusababisha uwiano wa vyeti vinavyofanana kuwa vigumu kutambulika. Hili linajitokeza katika viwango vya masaa ya kufundisha somo, mazoezi, na aina ya mitihani inayofanywa. Aidha tofauti hizi zinatokana na ukweli kuwa taasisi mbalimbali zinasimamiwa na secta mbalimbali za serikali au wafanya biashara ambao wanajali tu faida. Pia ukosefu wa viwango vya kitaifa kwa mitaala ya kozi zilizopo unachangia udhaifu huu.

**Pendekezo 5.3 :** Serikali iweke utaratibu wa kupanga na kusimamia viwango vya mitaala mbalimbali. Pia serikali iteue taasisi moja ambayo itakuwa na dhamana ya kusimamia mitaala katika taasisi za elimu ya juu za umma na watu binafsi. Hii itakuwa ni njia sahihi ya kutekeleza agizo la Rais Mhe. Jakaya Kikwete la kurekebisha mitaala.

**6. Umuhimu wa kuangalia kwa mapana athari za ongezeko kubwa la wanafunzi katika taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu**

**Hoja 6.1:** Pamoja na mazuri yaliyojitokeza ongezeko kubwa la wanafunzi katika vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu, ongezeko hili lina athari mbalimbali zikiwa ni pamoja na ukosefu wa wafanyakazi na wasaidizi wa kutosha, wafanyakazi na wasaidizi kukosa nafasi za kufundishia, ukosefu wa nyenzo za kufundishia masomo ya nadharia na mazoezi, wakufunzi kushindwa kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi mojamoja, wakufunzi kushindwa kuwatahini inavyopasa wanafunzi wao na mengine mengi. Kwa mfano vyuo vingi havina kumbi zinazoweza kuwachukua wanafunzi wote waliojisajili kwenye masomo mengine na hivyo wanafunzi wengi hubakia kuchungulia kwenye nyufa za kuta na madirisha. Aidha wakati wa mazoezi wanafunzi wengi wanabaki tu kuchungulia wenzao wakifanya mazoezi kwa kuwa nafasi ya kufanyia mazoezi ni finyu na vifaa vya kufanyia mazoezi ni vichache.

**Pendekezo 6.1:** Serikali itenge bajeti ya kutosha ya kukabiliana na athari za ongezeko kubwa la wananfunzi katika taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu kwa kufanya maboresho ya miundombinu, kuongeza mindo mbinu na vitendea kazi, kupanua au kujenga vyuo vipya vya kutosha kuajiri wanataaluma na wasaidizi wa kutosha.

**Hoja 6.2:** Ukosefu wa nafasi za ofisi umewafanya wafanyakazi wengi wa taasisi za elimu ya juu kufanya kazi zao za ofisi nyumbani na kutumia vyombo vya usafiri kama ndiyo sehemu za kuhifadhi nyaraka nyeti za kazini. wafanyakazi wengi wanafanya kazi kwa masaa mengi ya ziada kutokana na ongezeko la wanafunzi lakini hawalipwi kama taratibu za kazi zinavyoagiza. Aidha ukosefu wa vitendea kazi umewalazimu wafanyakazi wengi kugharamia mahitaji kama vile kalamu, karatasi, gharama za kudurufu, vitabu na machapisho mbalimbali ya kisayansi, na hata kompyuta na mitambo ya kikompyuta ya kufundishia kutokana na fedha ya mishahara wanayolipwa. Hii ina mantiki kuwa wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu wamekuwa ni wafadhili wakubwa wa elimu ya juu

na hili limefanya familia za wafanyakazi hao kukosa huduma bora kutokana na jasho lao.

**Pendekezo 6.2:** Serikali ijitahidi kutafuta gharama halisi za shughuli za ufundishaji na kutahini wananfunzi ili gharama hizi zibebwe na serikali badala ya kubebwa na wafanyakazi wa taasisi hizi.

**Hoja 6.3:** Ongezeko kubwa la wanafunzi linawafanya wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu wakose muda wa kufanya tafiti kama ilivyo ada ya wanataaluma wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu. Kutofanya tafiti kunaweza kuathiri kazi ya kuboresha mitaala na kubuni mbinu za kuyakabili matatizo ya kisayansi na kijamii.

**Pendekezo 6.3:** wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu wapewe ruzuku maalum na serikali itakayotumiwa kugharamia tafiti mbalimbali ambazo wafanyakazi hao wanahitaji kwa ajili kutatua matatizo ya kisayansi/kijamii na kuboresha mitaala.

7. **Umuhimu wa elimu ya utaifa kwa jamii ya Kitanzania**

**Hoja 7.1:** Katika kipindi cha utawala cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere juhudi za makusudi na za kudumu zilifanywa kujenga taifa imara kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile elimu ya watu wazima, makamisaa wa ideolojia ndani ya majeshi, Jeshi la kujenga Taifa, Mgambo, Chipukizi na vikundi vya nyimbo vya uhamasishaji ili kuhakikisha kuwa umma umeelimika katika mambo muhimu yanaoyohusu, utaifa, uzalendo, ulinzi, usalama na utamaduni wa raia. Sambamba na kuinua kiwango cha elimu ya kusoma na kuandika kufikia asili mia 80 (kuzidi nchi nyingine zote) utaratibu huo ulikuwa ndiyo saruji iliyounda taifa imara lenye msimamo, kuheshimika na lenye na amani na utulivu.

**Pendekezo 7.1:** Serikali irudishe na kuboresha utaratibu uliokuwepo hasa katika zama hizi za vyama vingi na utandawazi kwani kujenga uzalendo ndiyo njia kuu ya kuondoa uzembe kazini, na kudhibiti mfadhaiko unaoikumba nchi kwa ajili ya mauaji ya vikongwe, maalbino, ujambazi uliokithiri na ufisadi unaofanywa na viongozi ngazi mbalimbali za serikali na mashirika ya umma.

.

**Hoja 7.2:** Tafiti zinaonyesha kuwa wananchi sehemu mbalimbali za nchi hawana tena moyo wa kishiriki katika kazi za ujenzi na ulinzi wa taifa. Aidha maadili ya Viongozi, Watumishi na jamii kwa ujumla yameporomoka.

**Pendekezo 7.2.1:** Serikali itumie vyema taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu katika kutatua matatizo ya nchi badala ya kutumia wataalamu wa nje ambao hawajui mazingira halisi ya nchi na wala hawana sababu ya kulinda maslahi ya wananchi wa Tanzania. Serikali ionekane kuwa inatumia vyema kodi na mchango wa nguvu za raia katika maendelo ya nchi ili wananchi warudishiwe imani na moyo wa kujitolea katika shughuli za ujenzi wa taifa lao.

**Pendekezo 7.2.2:** Serikali iweke utaratibu wa kukabiliana na ongezeko kubwa la vyombo na taasisi za nje ambavyo/ambazo zina ushawishi mkubwa unaochangia kumomonyoa maadili ya raia ikiwa ni pamoja na majarida, filamu, programu za nje za luninga na radio ambazo hazina tija kwa usalama na maendeleo ya Taifa letu.

**Pendekezo 7.2.3:** Serikali iweke taratibu na mikakati ya kudumu ya kuwajenga wananchi wa Tanzania kisaikolojia kuwa wazalendo na wapiganaji hodari wa kutetea na kulinda uhuru wa taifa letu.

## 8. Umuhimu wa Watanzania kupunguza utegemezi na kurejesha moyo wa kujitegemea

**Hoja 8.1:** Kama alivyoinisha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere nchi hii ina maadui watatu wakuu, yaani Ujinga, Umasikini na Maradhi. Katika miaka ya sitini mpaka themanini serikali ilitumia rasilmali kubwa kupambana na maadui watatu wa nchi kwa mafanikio makubwa. Lakini baada ya mabadiliko ya kisiasia na kisera ya mwaka 1985/86 serikali ilipunguza sana matumizi ya bajeti katika vita hiyo. Matokeo ni kuongezeka kwa ujinga, umasikini na maradhi nchini.

**Pendekezo 8.1:** Serikali irejee sera za kujitegemea na imani za ujamaa zilizozaa matunda mazuri yaliyoleta maendeleo makubwa na kuimarisha uhuru wa jamii ya kiafrika miaka 25 ya mwanzo ya uhuru wetu. Iwekeze rasilmali kubwa katika vita ya kupambana na adui ujinga kwa kuchukua dhamana ya kuwapa elimu wananchi wake katika ngazi zote kwani watu wakishaelimika ni rahisi kuchangia kikamilifu kupambana na maradhi na umasikini.

**Hoja 8.2:** Historia inatufunza kuwa wale wakamata watumwa na wakoloni waliingia Afrika na mabara mengine kwa njia ya biblia na misahafu mingine ya dini. Serikali na wananchi wa Tanzania bado hawajaona hatari kubwa iliyoletwa na “dini” mpya ya “utandawazi” . Bado Watanzania wanautazama utandawazi kama ni changamoto ya maendeleo badala ya kuuona kama adui mkubwa wa maendeleo na hata maisha ya mataifa yote manyonge ya dunia. Kwa kadri rasilmali za dunia zinavyopungua ndivyo nchi zilizoendelea zitatumia dhana ya utandawazi kama shoka la kuvunja milango na kuingia nchini mwetu ili kupora kile wanachokihitaji. Hili tayari limejidhihirisha katika kuanguka uchumi wa nchi zilizoendelea jambo ambalo limechangiwa na matumizi yao mabovu ya rasilmali na uchumi wa dunia.

**Pendekezo 8.2:** Serikali ichukue hatua za kujenga upya vyama vya wakulima na wafugaji ambavyo vilishiriki kikamilifu kwaunganisha Watanzania na kuleta maendeleo ya kasi yaliyopatikana katika miaka ya mwanzo wa uhuru wa Taifa letu.

**Hoja 8.3:** Katika katiba za nchi nyingi swala la umiliki ardhi liko wazi – Haki ya kumiliki ardhi ni ya wananchi wazalendo/wazawa wa nchi husika tu. Lakini katika katiba yetu hili haliko bayana na isitoshe baada ya marekebisho madogo ya Katiba na Sheria ya Ardhi ya Mwaka 2004 iliyofanywa kwa ajili ya kuondoa “claw back clauses” katiba na sheria ya ardhi sasa “hazikatazi” mgeni yeyote kumiliki ardhi. Aidha wageni wengine wanatumia njia za panya kama vile “Watanzania vivuli”, “mikataba ya kumwoa Mtanzania/kuolewa na Mtanzania” ili kumiliki ardhi. TIC nayo imepewa mamlaka makubwa mno ya kugawa ardhi kwa kigezo cha kurahisisha uwekezaji wa makamupuni ya nje. TIC ikitumiwa kama dirisha la pili la kugawa ardhi imesababisha shuguli hii nyeti iwe na utata ambao sasa unazidi kujitokeza kadiri wananchi wanavyogundua kuwa ardhi yao imekwisha chukuliwa. Aidha TIC imekuwa ni kichocheo kikubwa cha “wajomba na mashangazi” toka nchi za nje ambao wanatumia kigezo cha kilimo cha “Biofuels” kukamata (“land grabbing”) maeneo

yenye ukubwa wa malaki hadi mamilioni ya hekta za ardhi katika maeneo nyeti ya kilimo, ufugaji, hifadhi na kadhalika.

**Pendekezo 8.3:** Serikali iwatumie wataalam na wananchi wa Tanzania kurejea na kutunga upya sera na sheria zote nyeti za nchi hii ili ziwe na sura na imani za Kitanzania ili tuweze kuzitumia kuimarisha uhuru na usalama wa nchi yetu na kwa njia hiyo tuvinusuru vitukuu vyetu na adha ya kuwa wakimbizi wasio na nchi katika bara la Afrika na Dunia kwa ujumla.

**Hoja 8.4:** Utegemezi mkubwa wa nchi yetu katika maswala ya kuunda sera na sheria zinazoongoza maendeleo yetu ni kansa inayolitafuna taifa na kupelekea kifo chake. Hili ni tishio kubwa kwani sera na sheria za nchi zinatakiwa zitokane na imani juu mahusiano ya wananchi na ardhi, wananchi na viongozi wao, na mahusiano ya kibiashara, kidini, kitamaduni, kijamii na kadhalika katikati yao. Anapochukuliwa mtaalam toka nchi nyingine kuunda sera au sheria ni wazi sera na sheria anazozitunga zitachukua sura ya nchi anakotoka na hazitakuwa na misingi ya Kitanzania.

**Pendekezo 8.4:** Serikali ilichukulie **s**wala la ardhi kwa ajili ya "biofuels" kama swala nyeti la kiusalama na ichukue hatua za dharura kuweka kikomo ("moratorium") katika swala la kutoa ardhi kwa ajili ya kilimo cha "biofuels" mpaka hapo wataalam wetu wenyewe watakapotafiti ukweli juu ya faida na athari za "biofuels". Serikali itafiti kwanza athari za kutoa maeneo makubwa kupita kiasi kwa uhuru na usalama wa vizazi vijavyo vya Watanzania. Aidha Serikali irejeshe maeneo yote ambayo yalichukuliwa tayari ilhali serikali haijaweka sera ya kilimo cha "biofuels" na iweke utaratibu mpya wa wananchi wazalendo kuchukua maeneo hayo kama itaonekana "biofuels zina maslahi kitaifa.

**9. Hitimisho**

Hoja na mapendekezo mengine yaliyotolewa na chama hiki yanahitaji tafiti zaidi ili serikali iweze kufanya maamuzi juu ya hoja na mapendekezo hayo kwa kutumia takwimu zinazokubalika. Chama cha THTU kiko tayari kushirikiana na serikali kufanya tafiti hizo ili serikali iweze kutoa ufumbuzi wa kudumu wa matatizo ndani ya jamii. Mwisho uongozi wa chama hiki kipya unamshukuru Waziri Mkuu na Serikali yake kwa mwaliko huu wa maongezi Ofisini kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**NIA NA MWELEKEO WETU DAIMA NI KUJENGA.**

**9. Viambatanisho**

**9.1 Jedwali 1 : U**linganisho wa mishahara mwaka 2004 na mapendekezo ya 1994

**9.2 Jedwali 2: M**apendekezo ya mishahara ya kuanzia ya mwaka 2004

**9.3 Jedwali namba 6: G**harama za kuongeza mshahara kwa kila chaguzi

**9.4 Kiambatanisho namba 5:** Mchanganuo wa mahitaji ya nyongeza za mishahara kwa waendeshaji wa vyuo vikuu

**9.5 Jedwali :** Hatua za kuchukua kuboresha mazingira ya kufanya kazi wanataaluma wa vyuo vikuu

**9.6 Table 6** : Tanzania social security (pension) funds – benefits scenarios

**9.7 Agenda No. 1** ya tarehe 2/August/2008 ya Kikao cha Kamati ya Viongozi wa Vyuo Vikuu vya Umma: Taarifa ya Mchanganuo wa Utekelezaji wa Mishahara ya Wafanyakazi Waendeshaji.

**JEDWALI NAMBA 1:** ULINGANISHO WA MISHAHARA YA MWAKA 2004 NA MAPENDEKEZO YA MWAKA 1994

| **Ngazi ya Mwanataaluma** | **Mshahara wa 2004** | | **Mapendekezo ya 1994 ya mshahara wa kuanzia** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Shs/Mwezi** | **Dola/Mwezi** | **1994* Dola/Mwezi** | **2004** Shs/Mwezi** |
| Profesa | 1,052,330 | 915.07 | 1,680.95 | 1,933,092 |
| Profesa Mshiriki | 870,4800 | 756.94 | 1,563.50 | 1,798,025 |
| Mhadhiri Mwandamizi | 726,070 | 631.36 | 1,446.04 | 1,662,946 |
| Mhadhiri | 489,390 | 425.56 | 1,328.59 | 1,527,878 |
| Mhadhiri Msaidizi | 368,010 | 320.00 | 1,115.58 | 1,282,917 |
| Mkufunzi Msaidizi | 282,360 | 245.53 | 998.12 | 1,147,838 |
| * Mapendekezo ya 1994 – Dola moja = Shs 550<br>** Mapendekezo ya mshahara ya 1994 kwa kuzingatia kuporomoka kwa thamani ya shilingi – (2004 – Sola 1 = Shs 1,150) | | | | |

**JEDWALI NAMBA 2:** MAPENDEKEZO YA MISHAHARA YA KUANZIA YA MWAKA 2004

| **Ngazi ya Mwanataaluma** | **Mshahara wa 2004** | | **Mapendekezo ya 1994 ya mshahara wa kuanzia** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Shs/Mwezi** | **Dola/Mwezi** | **1994* Dola/Mwezi** | **2004** Shs/Mwezi** |
| Profesa | 1,052,330 | 915.07 | 1,976.55 | 2,273.030 |
| Profesa Mshiriki | 870,4800 | 756.94 | 1,634.99 | 1,880,240 |
| Mhadhiri Mwandamizi | 726,070 | 631.36 | 1,363.75 | 1,568,310 |
| Mhadhiri | 489,390 | 425.56 | 919.20 | 1,057,080 |
| Mhadhiri Msaidizi | 368,010 | 320.00 | 691.22 | 794,900 |
| Mkufunzi Msaidizi | 282,360 | 245.53 | 530.35 | 609,900 |
| * Mapendekezo ya 1994 – Dola moja = Shs 550<br>** Mapendekezo ya mshahara ya 1994 kwa kuzingatia kuporomoka kwa thamani ya shilingi – (2004 – Sola 1 = Shs 1,150) | | | | |

**JEDWALI NAMBA 6:** GHARAMA ZA KUONGEZA MSHAHARA KWA KILA CHAGUZI

| Namba | Cheo | Ngazi ya Mshahara | Mshahara kwa Sasa | Mshahara Unaopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Scenario 1 | Scenario 2 | Scenario 3 |
| 1 | Professor | PHTS 21 | 1,309,800 | 2,273,030 | 2,032,220 | 1,791,420 |
| 2 | Assoc Prof | PHTS 19/20 | 1,177,710 | 1,880,240 | 1,701,610 | 1,528,060 |
| 3 | Senior Lecturer | PHTS 17/18 | 934,620 | 1,588,310 | 1,400,890 | 1,251,470 |
| 4 | Lecturers | PHTS 15/16 | 670,440 | 1,057,080 | 960,420 | 863,760 |
| 5 | Assistant Lecturer | PHTS 13/14 | 485,280 | 794,000 | 717,500 | 640,090 |
| 6 | Tutorial Assistant | PHTS 12 | 370,160 | 606,990 | 549,900 | 490,030 |

**JEDWALI :** HATUA ZA KUCHUKUA KUBORESHA MAZINGIRA YA KUFANYA KAZI WANATAALUMA WA VYUO VIKUU

| **Na.** | **Maelezo** | **Gharama** |
|---|---|---|
| 1. | Kujenga na kukarabati miundombinu | 28,942,817,214 |
| 2. | Kuboresha mifumo ya mawasiliano na vifaa vya ICT | 2,459,976,000 |
| 3. | Kukarabati na kuboresha huduma za maktaba | 10,933,100,000 |
| 4. | Kujenga hosteli za kulala wananfunzi | 7,200,132,831 |
| 5. | Kulipa madeni ya wanataaluma | 1,020,442,000 |
| 6. | Kujenga ofisi za wanataaluma | 6,069,500,000 |
| 7. | Kukarabati na kuboresha mifumo ya maji, simu, na umeme | 1,773,000,000 |
| 8. | Kukarabati nyumba za wafanyakazi | 550,000,000 |
| | **JUMLA** | **58, 948, 968,045** |

**Table 6 : TANZANIA SOCIAL SECURITY (PENSION) FUNDS – BENEFITS SCENARIOS**

| Parameter | GEPF | SSSS | PPF | PSPF | NSSF | LAPF |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Period of Service, PS = 25 yrs (300 months) since 1984** | | | | | **Average Gross Monthly Salary =** | **1,500,000** |
| PS [months] | -- | -- | 300 | 300 | 300 | 300 |
| PF | -- | -- | 1/960, 1/600 | 1/540 | (1/720 .... 1/600) | 1/540 |
| CF [years] | -- | -- | 12.5 | 15.5 | 18 ***(12.5 for Total MP)*** | 15.5 |
| Basis | -- | -- | APE | LMS-A, SA | AME | LMS-A, SA |
| Basis Amount [TShs] | -- | -- | 18,000,000 | 10,000,000 | 1,500,000 | 10,000,000 |
| CPG [TShs] | -- | -- | 26,015,625 | 77,500,000 | 36,000,000 | 77,500,000 |
| MP [TShs] | -- | -- | 520,313 | 416,667 | 675,000 | 416,667 |
| Total MP for CF [TShs] | -- | -- | 78,046,875 | 77,500,000 | 101,250,000 | 77,500,000 |
| **Total Pension [TShs]** | -- | -- | **104,062,500** | **155,000,000** | **137,250,000** | **155,000,000** |
| Minimum - Maximum Allowed Monthly Pension (MP) | -- | -- | Minimum * 21,000/- Maximum 2/3 of HMS | -- | Minimum 30% AME Maximum 67.5% AME | No Limits |
| Gratuity (Max) for PS less than 10 or 15 yrs | Total Contributions | Purchased Benefit | 41,625,000 | 46,500,000 | 36,000,000 | 5 x SA = 50,000,000 |
| Disability / Invalidity | -- | -- | CPG plus MP for life | CPG plus MP | CPG + (30+1)% AME | CPG plus MP or Gratuity |
| Death (Member's) | -- | -- | CPG or APE | CPG | MP x 12 months | CPG plus MP or Gratuity |
| Funeral Grant | -- | -- | *NIL* | *Not Specified* | *Board to determine* | *Not YET specified* |
| Survivors'/Dependants | -- | -- | MP x 36 months | MP x 36 months | MP for "life" or 2 years | MP x 36 months |
| Withdrawals-1: Marriage, Maternity and/or Sickness | -- | -- | -- | -- | 6 x 5% of Members' Total Contributions | Total Contributions plus Interest (10%) |
| Withdrawals-2: Emigration and/or Unemployment | -- | -- | Total Contributions | Total Contributions | -- | Total Contributions plus Interest (10%) |
| Others | -- | -- | **Education** | -- | **Health Insurance** | Adv. 50% of CPG |

Source: Prof Magembe's Pension Funds Report of 2008, see Key below.

**Key:** APE = Annual Pension Emolument (PPF), AME = Average Monthly Earnings (NSSF), CF = Commutation Factor
CPG = Commuted Pension Gratuity (PPF), GB = Gratuity Benefit (PPF), HMS = Highest Monthly Salary (PPF)
LAS = Last Annual Salary (PSPF, LAPF), MP = Monthly Pension, PF = Pension Factor (PPF, PSPF, LAPF)
PS = Period of Service, SA = Specified Amount (PSPF, LAPF)